# STD 5 MID TERM 2, 2017
# KISWAHILI

***Chagua jibu sahihi kuanzia swali la 1-15.***

Mlango __1__ mwalimu __2__ Kiswahili __3__ aliyekuwa wa __4__ kuingia katika darasa __5__ la tano. Kipindi __6__ asubuhi kilikuwa __7__. Alitusabahi kama __8__ desturi __9__. Baada ya shughuli za hapana pale darasa __10__ Alianza kutueleza __11__ kuandika hati safi __12__ darasani, __13__ pia maishani __14__. Kisha alituita __15__ ubaoni tukaandika neno hati.

**1.** A. ulipofugwa B. ulifunguliwa C. ulipofunguliwa D. ulipofungulia

**2.** A. ya B. kwa C. cha D. wa

**3.** A. ndio B. ndivyo C. ndiye D. ndiyo

**4.** A. kuanza B. kuwanza C. kwaza D. kwanza

**5.** A. letu B. yetu C. mwetu D. kwetu

**6.** A. ile ya B. kile cha C. hiyo ya D. hii ya

**7.** A. yake B. lake C. wake D. chake

**8.** A. iliyokuwa B. lilivyokuwa C. ilikuwa D. ilivyokuwa

**9.** A. yetu B. kwake C. yake D. wetu

**10.** A. ule B. lile C. zile D. ni

**11.** A. jinsi ya B. hali ya C. vile ya D. nini ya

**12.** A. siku tu B. siyo tu C. siotu D. siye tu

**13.** A. mbali B. pale C. bali D. vile

**14.** A. yetu B. mwetu C. zetu D. wetu

**15.** A. moja B. mmoja C. mojawapo D. mmoja mmoja

***Chagua jibu sahihi***

**16.** Jua kali ni la __________
A. utasa B. utasa C. utesi D. utosi

**17.** Kazi yake ni _______
A. zuri B. mzuri C. kizuri D. nzuri

**18.** Ganda la ugali linalobakia chini ya chungu ni ______
A. ukoka B. ugaga C. ukoko D. utando

**19.** Masika ________ mwomba mwalimu Tunoi ruhusa alipotoka.
A. haja B. hange C. haku D. hata

**20.** Kitanda kina matendegu ilhali gari lina _______
A. magando B. miguu C. usukani D. magurudumu

**21.** Alikuja a _____niambia nimpe wali ale.
A. li B. ta C. me D. ka

**22.** Maiti _______ kesho.
A. hii atazikwa B. hii itazikwa C. huyu atazikwa D. huyu itazikwa

**23.** Mgonjwa alipewa ________ kunywa.
A. madawa ya B. dawa za C. vidonge za D. tembe vya

**24.** Sisi ________ na vitabu tunsoma nini?
A. tusio B. tusiyo C. tusivyo D. tusiye

**25.** ***Andika kwa wingi***
Mtoto wako atakufungia chumba chako.
A. Watoto wao watawafungia nyumba zao.
B. Watoto wako watakufungia vyumba vyako
C. Watoto wenu watawafungia vyumba vyenu
D. Watoto wenu watawafungia vyumba vyenu.

**26.** Swali la mwanafunzi lilikuwa ______ na _______
A. njema, nzuri B. jema, mzuri C. jema, nzuri D. jema, zuri

**27.** Msemo tuling'oa nanga unamaanisha _________
A. tulianza safari B. tulitoroka C. tulibeba nanga D. tulikimbia

**28.** Chagua sentensi yenye matumizi mabaya ya -amba
A. Chakula ambacho nimekila ni kitamu
B. Watu ambao waliokuja kwetu ni wageni
C. Magari ambayo tunayo ni mapya
D. Mwanafunzi ambaye husoma hufaulu

**29.** Vikombe 12 kwa maneno ni _________
A. vikombe kumi na mbili
B. vikombe kumi viwili
C. vikombe kumi na viwili
D. vikombe vikumi na viwili

**30.** Simba ________ swara hadi msituni.
A. alimkimbiza B. alikimbisha C. aliikimbia D. alizikimbia

***Soma habari hii kisha ujibu maswali 31-40.***

Vijiji vya Gatuzi vimebaki kama visiwa na wakazi wote hawawezi kuondoka kwenda mahali popote kwa sababu ya kuzingirwa na mafuriko.

Tangu mvu kubwa ianze kunyesha sehemu zote, wananchi hawajapokea misaada yoyote ya usafiri, vyakula wala dawa za kujikinga na kujitibu kutokana na magonjwa kama vile kichocho, malaria, homa ya matumbo na kuhara. Kwa muda mrefu sana mvua kubwa imekuwa ikinyesha katika magatuzi yote ya nchi yetu.

Kulingana na maelezo ya wataalam wa hali ya mazingira, mafuriko hayo yamesababishwa na hatari za kuharibu mazingira kote nchini. Watu wanakata miti ovyo ovyo na kulima kila sehemu. Hawajui kwamba mizizi ya miti hiyo ndiyo inayoshikilia udongo na kuzuia mmomonyoko. Pia watu wengine wanalima hadi kando

kando ya mito na kusababisha kuwepo kwa udongo laini karibu na kingo za mto.

Tatizo jingine ni kujenga kila mahali bila kuyajali mazingira. Wakati umefika ambapo lazima tuyatunze mazingira vizuri. La sivyo, majanga yatakuwa mengi. Na janga ni jangamizi, huangamiza.

31. Vijiji vimebaki kama visiwa kwa sababu:-
A. ya kuzungukwa na mafuriko
B. wakazi hawawezi kutoka
C. hawajapokea misaada
D. hakuna dawa

32. Tangu mvua iaanze kunyesha ______
A. wakazi wamekata miti B. magonjwa yamezidi
C. hakuna magonjwa D. wataalam wamekuja

33. Mvua kubwa imekuwa ikinyesha kwenye _______
A. baadhi za wilaya B. vijiji vingine
C. kila gatuzi D. sehemu fulani za nchi

34. Wataalam wa mazingira wanasema _______
A. mafuriko ni hatari
B. watu wanakata miti
C. mvua itazidi
D. uharibifu wa mazingira ni hatari

35. Mizizi ya miti _____
A. husaidia kushikilia udongo usimomonyoke
B. husababisha mafuriko karibu na mito
C. husababisha udongo kuwa laini
D. ni dawa ya tumbo

36. Tunaambiwa kwamba watu wengine wanalima ____
A. kwenye mito B. karibu sana na mito
C. mazingira ya mto D. kutoa mizizi

37. Tuyatunze mazingira ili ______
A. tujenge mbali na mto B. kuzuia udongo
C. kuzuia janga la mafuriko D. tusilime

38. Mara nyingi mafuriko hutokea nyakati za ______
A. masika B. kiangazi C. vuli D. kipupwe

39. Katika taarifa hii neno <u>**wakazi**</u> lina maana ya watu ambao ni:-
A. wafanyakazi B. wana kazi
C. wenyeji D. wa kazi

40. Taarifa hii ni kuhusu janga la _______
A. mazingira B. mafuriko
C. miti D. magonjwa

***<u>Soma kara hii kisha ujibu maswali 41-50.</u>***

Mimi hupenda mchezo wa kandanda. Sijui wewe hupenda mchezo gani. Lakini licha ya kupenda mchezo huo, siwezi kukosa usingizi ati kwa sababu timu fulani imeshindwa au imeshinda. Sina uzembe wa sampuli hiyo. Kandanda hunifurahisha lakini si hunipumbaza na kunilevya kuniteka bakunja hadi nikawa mbumbu mzungu wa reli. La hasha!. Wachezaji wa soka wanapocheza, hufanya kazi yao. Nami nikiwa na kazi yangu siachi kufanya nikazama katika kazi ya mtu mwingine.

Ninajua na kuelewa kuwa wapo mashabiki ambao mpira ukianza dakika tisini hawana kazi ila kukodoa macho ama kushangilia. Mwishoni, timu anayoishabikia ikishindwa hakuli, ikishinda halali. Kila ulevi ni hatari. Ulevi wa mpira pia una matata yake. Lakini hivyo ndivyo mambo yalivyo. Kipendacho moyo ni dawa.

Juzi, timu yangu niipendayo iliingia ugani kuchuana na timu nyingine. Pambano lilikuwa kali kiasi cha nyasi kuumia na mashabiki roho mikononi. Baada ya kipindi cha awali, kipenga kilipulizwa, timu zote zikawa sare tasa. Kipindi cha pili, upepo ulianguka. Kunako dakika ya themanini na tano, timu niipendayo ifafunga bao. Wavu ulipotikiswa, moyo wangu ulisikitika na kusikitika kidogo tu. Labda ningekuwa wewe, ningezirai. Ilipowadia dakika moja tu tisini zitimie, mchambuliaji alitia bao kimiani. Matokeo yakawa sare ya bao moja kwa moja. Huko ndiko kunusurika na kuponea katika tundu la sindano.

41. Kandanda ni mpira wa _________
A. pete B. wavu
C. miguu D. magongo

42. Msemaji hakosi usingizi _________
A. timu zinapocheza
B. kwa kupenda kandanda
C. timu yake ikishindwa
D. kwa matokeo ya kandanda

43. Mzungumzaji wa habari kwa hakika _______
A. hapendi kabisa kandanda
B. ni shabiki sana
C. hupenda kandanda lakini kwa uangalifu
D. haungi mkono kandanda

44. Uzembe wa watu wengine ni kwamba ________
A. haucha kazi zao wakati wa kandanda
B. hawana timu yoyote
C. hawapendi wachezaji wa timu nyingine
D. huwashabikia wachezaji au wanakandanda

45. Mchezo wa kandanda huchezwa na watu wangapi uwanjani?
A. Wachezaji ishirini na wanne
B. Wachezaji ishirini na wawili
C. Wachezaji ishirini
D. Wachezaji kuni na mmoja

46. Sare zinazovaliwa na wanakandanda ________
A. jezi na buka B. mashati na suruali
C. fulana na ndengirizi D. mashatitao na kaptura

47. Juzi msimulizi __________
A. alicheza kandanda B. alishabikia timu yake
C. alikosa usingizi D. aliona nyasi zikiumia

48. Timu zilizocheza hatimaye _________
A. zilienda sare tasa B. zilitoka sare
C. zilipigana D. hazikutia bao lolote kimiani

49. Timu iliyoponea chupuchupu ni ________
A. aliyoshabiki msemaji B. iliyotikisa wavu
C. yenye tundu la sindano D. iliyoshinda nyingine

50. Taarifa hii inatufundisha kwamba:-
A. kandanda ni mbaya
B. mashabiki wajue kwamba asiyekubali kushindwa si mshindani
C. tushabikie timu zote
D. timu zote huwa sare